JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA
CHUO CHA UALIMU KLERRUU

SIMU: 026-2702804/2701631

Barua pepe : klerruutc@gmail.com

Chuo cha Ualimu Klerruu
S.L.P 549,
IRINGA.

Fax Na. 026-2701631 IRINGA.

Kumb. Na. KLERCU/TV48/…….. 03 /07/2020

JINA

……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA MAALUMU (ELIMU YA SAYANSI), STASHAHADA YA SAYANSI ELIMU YA SEKONDARI KWA MASOMO YA SAYANSI 2020/2021.

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na mafunzo ya Stashahada katika chuo hiki kwa mwaka wa masomo 2020/2021. Hii ni nafasi muhimu kwako itakayokuwezesha kuwa mwalimu aliyekidhi vigezo kitaaluma. Hivyo ninakupongeza sana. Kufika chuoni kwa muda muafaka kutakupa nafasi ya kushiriki katika mafunzo kabirishi ya kukifahamu chuo zaidi.

Unatakiwa kusoma kwa umakini na kuelewa maelekezo yote ya kujiunga na mafunzo na pia kuripoti chuoni kwa muda muafaka. Endapo utashindwa kuripoti kwa muda uliopangwa ikipita WIKI MOJA nafasi yako atapewa mtu mwingine.

Wazazi/Walezi/Waajiri na wanafunzi watatakiwa kujaza fomu ya makubaliano iliyoambatanishwa kwenye fomu hii na kuwasilishwa kwa msajili wakati wa usajiri. Kila Mwanachuo atapaswa kufanyiwa vipimo vya afya na kuleta fomu ya majibu ya daktari.

1. KUFUNGUA

Muda kuripoti ni tarehe **24/08/2020 – 07/09/2020** kwa wanachuo wa Stashahada maalumu ya Sayansi mwaka wa kwanza na kwa Stashahada ya Sayansi elimu ya sekondari ni tarehe **01/10/2020 – 14/10/2020.** wanafunzi wote wanatakiwa kuripoti chuoni kabla ya **Saa tisa na nusu alasiri**. Mafunzo kabirishi ni muhimu kwa wanachuo wote na yataanza mapema mara tu baada ya chuo kufungua.

2. TAARIFA ZA CHUO KILIPO

Chuo cha Ualimu Klerruu kipo katika Manispaa ya Mkoa wa Iringa; ni karibu kilomita 1.5 toka ofisi za Makao makuu ya Posta mkoa wa Iringa pembezoni mwa barabara ya Dodoma. Mkoa wa

Iringa ni rahisi kufikika toka mikoa ya Dodoma, Rukwa, Mbeya, Morogoro/Dar es Salam kwa usafiri wa mabasi.

3. KAULIMBIU YA CHUO

UFAHAMU NA USTADI NI UHURU

4. KOZI ZITOLEWAZO NA MUDA WAKOZI

- Stashahada Maalumu ya Elimu Sekondari (Sayansi) – Miaka 3
- Stahahada ya Elimu Sekondari (Sayansi) - Miaka 2

4.3. YAHUSUYO KOZI

Kwa ujumla mafunzo ya ualimu yanahusisha shughuli za kimtaala na zisizo za kimtaala katika mfumo wa; Mihadhara, Semina, Mazoezi ya kufundisha kwa vitendo, Utunzaji wa mazingira pamoja na Michezo mbalimbali.

4.3.1. MAHITAJI YA MUHIMU YA KOZI

Kila mwanachuo atapaswa kufika katika ofisi ya Msajili na vitu vifuatavyo:

- Nakala mbili za muhtasari wa elimu ya sekondari kwa masomo atayosomea.
- Seti ya vifaa Hisabati (kwa wale wa mchepuo wa Hisabati).
- Vitabu vya kiada (hususani vitabu maalumu kwa masomo ya kufundishia shule za sekondari).
- Daftari kubwa zisizipungua kumi (10).

4.3.2. MAVAZI/VIFAA YA MICHEZO

Kila mwanachuo atapaswa kushiriki katika michezo kwa kuzingatia ratiba ya chuo, na atatakiwa kuja na vitu vifuatavyo kwa ajili ya michezo:

1. Trakisuti — Rangi ya “dark blue”
2. Fulana nyeupe
3. Kaptura ya “dark blue”
4. Sketi ya “dark blue”
5. Viatu vya mazoezi
6. Soksi nyeupe zenye ufito wa rangi ya bluu.

4.3.3. SARE ZA CHUO

Sare za chuo chetu ni kama ifuatavyo:

-

- Suti pea mbili— “dark blue” (koti + suruali/sketi Mbili + tai)
- Mashati mawili ya mikono mirefu rangi ya bluu bahari
- Viatu vya ngozi vya Kamba, rangi nyeusi.
- Koti jeupe la maabara la mikono mirefu (kama la madaktari)

Sare ziwe kama muonekano unaoonekana pichani





- Sketi iwe ya heshima urefu unaovuka magoti
- Suruali iwe ya heshima yenye upana chini inchi 16

MUHIMU: Endapo rangi na mshono hutauelewa fanya mawasiliano chuono kwa maelekezo zaidi.

- Fulana yenye nembo ya Chuo 15,000(Itapatikana chuoni)

5.0 UTAMBULISHO NA VIGEZO VYA KITAALUMA

Kila mwanachuo anayeripoti chuoni lazima alete

- Barua ya kujiunga na mafunzo na fomu ya kujiunga na mafunzo
- Nakala za matokeo ya awali (Result slips) zitapokelewa tu kwa wanzafunzi waliomaliza kidato cha nne mwaka 2019 na wa kidato cha sita waliomaliza mwaka 2020.
- Cheti cha uchunguzi wa afya (Medical Examination Certificate) kilichothibitishwa na kupigwa muhuri na afsa afya wa wilaya au afisa afya mkoa.
- **Vyeti halisi** (**sio Nakala**) vya kidato cha nne na kidato cha sita , pamoja na cheti cha kuzaliwa.

ZINGATIA. Toa Nakala nyingi za yeti hivyo ubaki nazo kwa matumizi binafsi.

5.1. UCHANGIAJI WA GHARAMA

5.1.1. ADA

Mwanachuo atahitajika kulipa ada ya kiasi cha Shilingi **450,000** /= kwa kila mwaka wa masomo. Kiasi hicho kitatakiwa kulipwa kwa mkupuo mara moja kwa mwaka au kulipwa kwa mafungu mara

mbili kwa mwaka wa masomo kwa kila mwanzo wa muhula (**225,000/=**). Usipokuja na kiasi tajwa hapo juu hutopokelewa chuoni. Malipo ya ada yatahitajika kulipwa kwa kutumia mfumo wa malipo serikalini (GEPG)

baada ya kupata namba ya malipo **(CONTROL NUMBER)** kutoka kwa mhasibu wa Chuo mara baada ya kuwasili chuoni. Mwanachuo atatakiwa kuwasilisha nakala ya benki ya malipo ya ada (Bank pay-in slip) kwa ajili ya hatua za usajili.

5.1.2 MICHANGO MINGINE

- Mchango wa Serikali ya wanachuo sh. 5,000 (kwa mwaka)
- Huduma ya kwanza sh.10,000 (kwa mwaka)
- Michezo sh.30,000/= (kwa mwaka)
- Kitambulisho na usajili sh.20,000 (Mara moja)
- Mchango wa mahafali utatangazwa muda ukifika kwa kuzingatia mahitaji ya wakati husika
- Usafi na utunzaji mazingira sh. 20,000(Kwa mwaka)
- Ulinzi sh. 30,000 (Kwa mwaka)
- Matengenezo sh.25,000 (kwa mwaka)
- Godoro sh. 10,000 (kwa mwaka)
- Utakapofika mwaka wa pili utatakiwa kulipa **ada ya mtihani** kulingana na viwango vya Baraza la Mitihani kwa wakati huo.

Malipo yote ya michango yatatakiwa kulipwa kwa kupitia benki ya **NMB** Mkwawa kwa akaunti namba **60501100006** jina la akaunti **Principal Klerruu T.C**. Mwanachuo atatakiwa kuwasilisha nakala ya malipo wakati wa usajili. Michango yote ni ya lazima.

MUHIMU: Usichanganye ada na michango katika akaunti hii.

52.3. HUDUMA ZA AFYA NA MALAZI

Kila Mwanachuo atahitajika kuja na vitu vifuatavyo kwa matumizi yake binafsi kwa ajili ya huduma za malazi na chakula: Mashuka ya kutandika kitandani rangi ya bluu(kwa wavulana) na rangi ya pinki (kwa wasichana), blanketi, chandarua, pamoja na mto na foronya yake. Magodoro yanapatikana chuoni kama iliyoanishwa kwenye sehemu ya michango. Pia utatakiwa kununua pazia rangi ya pink (msichana) na bluu (mvulana) pamoja na mishikio yake, ukubwa wa dirisha la chumba ni futi 3x6.

Vitu vifuatavyo ni muhimu pia kuja kuwa navyo: Ndoo, sahani ya chakula, bakuli,kikombe. Pia uwe na chupa kubwa/kidumu cha kuhifadhia maji ya kunywa yaliyochemshwa.Unashauriwa kuja na fedha kwa ajili ya matumizi binafsi. Chuo hakitoi mlo maalumu kwa mwanachuo yeyote.

ZINGATIA: Wanachuo wa kike wa dini ya kiislamu wataruhusiwa kuvaa vazi la "HIJAB" rangi ya bluu bahari.

6.0. KANUNI NA SHERIA ZA CHUO

- Kanuni na sheria za chuo mwanachuo atazipata chuoni wakati wa mafunzo kabirishi.

Tunakutakia kila la kheri katika maandalizi ya kujiunga na chuo chetu.

Karibu sana,

……
TUMAINI A MANGILIMA
MKUU WA CHUO

WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA
CHUO CHA UALIMU KLERRUU

FOMU YA MAKUBALIANO: KUKUBALI KANUNI ZA KUJIUNGA NA CHUO

Kwa Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Ualimu Kleruu,
S.L.P 549,
Iringa.

SEHEMU 1: 1--111 IJAZWE NA MWANACHUO
Ahsante kwa barua Kumb,Na KLERCU/GFO/VOL.II ya tarehe.....
Ikinifahamisha kuwa nimechauliwa kujiunga na chuo cha Ualimu Klerruu kusomea Stashahada ya Ualimu wa Sekondari (Sayansi)/ Stashahada maalumu ya Sayansi.

Mimi _____ (Jina kamili), ninapenda kukujulisha kuwa nipo tayari kujiunga na chuo cha Ualimu Klerruu, na;

a. Nimesoma na kuelewa mahitaji yote kama yalivyoainishwa kwenye masharti ya kujiunga na chuo.
b. Nina ahidi kufuata na kutekeleza yote yaliyoainishwa kwenye maelekezo ya kujiunga na chuo. Ninatambua kuwa kushindwa kutekeleza hayo, nitawajibika na kukubali hatua za kinidhamu ambazo zitachukuliwa dhidi yangu.
c. Nina ahidi kushiriki ipasavyo katika shughuli za kitaaluma kama vile: kuhudhuria darasani, mazoezi, kazi za darasa, majaribio, na mitihani na kazi za nje ya darasa kama vile: michezo na shughuli zingine itakapobidi.
d. Nina ahidi kutenda na kuonesha tabia njema ndani ya chuo na kuwa mfano wa kuigwa katika jamii kwa kufuata sheria na taratibu za kazi ya Ualimu.
e. Nina ahidi kufika chuoni kwa tarehe za kufungua chuo zitakavyoonesha na kuleta mahitaji yote muhimu.
f. Nitarudi kwa wazazi/walezi/muajiri wangu kipindi cha likizo kwa anuani ifuatayo:
   Jina.....
   Anuani.....
   Wilaya.....
   Mkoa .....
   Simu.....

Saini ya Mwanachuo_____ Tarehe .....

SEHEMU 11: MZAZI/MLEZI MUAJIRI

Mimi _____ (Jina kamili) ni mzazi/mlezi/muajili wa(Jina kamili la Mwanachuo).

1. Ninathibitisha kuwa Mwanachuo alichaguliwa yupo Chini ya usaidizi na uangalizi wangu. Ninakubali ya yote aliyoahidi kufata. Nina ahidi kutoa msaada wa hali na mali kwa ajili ya kumsaidia kufanya vizuri katika masomo yake.
2. Nina ahidi kwamba Mwanachuo huyu atapata mahitaji yote ya Vitu na fedha(Ada) ili kumuwezesha kusajiliwa na kumaliza mafunzo yake.
3. Nina ahidi kushirikiana na Uongozi wa chuo na jamii katika kumuwezesha Mwanachuo huyu kuwa na tabia na maadili mema yanayoenda na taaluma ya Ualimu.
4. Nitashirikiana na Uongozi wa chuo na jamii nzima katika kuchukua hatua stahiki katika kujengea Mwanachuo tabia njema katika nja sahihi.

Jina.....

Anuani.....Namba ya simu ya mezani.....

Simu……../ ……. Barua pepe ……. Wilaya ……. Mkoa ……

GOVERNMENT OF TANZANIA

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM

THE PRICIPAL,
KLERRUU TEACHERS' COLLEGE, P.O.BOX 549,
IRINGA.

DATE.....

TO: The Medical Office,

_____

RE: MR/MRS/MISS

.....

(Name if Full)

Please examine the above as to his/her physical and mental fitness for a full time teacher — training course.

The examination should include the following categories (I — Il) each category or sub — category of which will render the applicant ineligible in case of defect. Pregnancy (category IV) will also render a girl candidate ineligible for the course including

(a) Eye sight

(b) Hearing

(c) Limbs

(d) Speech

(e) Neuroses

(Il) Pregnancy

(Ill) Mental and physical fitness

(IV) Venereal disease

(f) Leprosy

(g) Peptic ulcers

(h) Epilepsy

(i) Tuberculosis

PART B

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally

(a) Eye — sight ……

(b) Hearing……. .

(c) Limbs ……

(d) Speech. ..……

e) Venereal Disease.…

(Il) Neurosis.... . . . .

(Ill) Other serious disease……...

(IV) Mental and physical fitness……

(f) Venereal disease……

(g) Leprosy…….

h) Peptic Ulcers…….

(i) Epilepsy……

(j) Tuberculosis……

fit/unfit for full time teacher training course.

Date……Signature……..Designation……

Station …… Official Stamp. . ……..